HOTUBA YA WAKALA WA BARABARA (TANROADS) KWA WANACHAMA WA UMMA WA WAPANDA BAISKELI DAR ES SALAAM (UWABA)

09 MEI 2010

Mheshimiwa Mgeni Rasmi

Ndugu Wanachama wa UWABA

Ndugu Wageni Waalikwa

Ndugu Mabibi na Mabwana

Kwa niaba ya Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS), napenda kuwashukuru sana Nchi za Umoja wa Ulaya (European Union) kwa kutualika katika hafla hii ya msafara wa baiskeli ulioandaliwa kwa pamoja na Umma wa Wapanda Baiskeli (UWABA).

Binafsi nikiwa mshiriki sana na mpenda mazoezi, imekuwa ni fursa tena kushiriki tukio ninalolithamini sana. Ninatoa rai ushirikiano huu uliobainishwa kwa mwaliko wa UWABA na Umoja wa Ulaya kwa TANROADS usiishie hapa bali uendelee zaidi, lengo likiwa ni kuhamasisha matumizi ya baiskeli kwa usafiri wa kila siku kwa usalama, kujiamini na raha.

TANROADS tunashiriki katika msafara wa wapanda baiskeli kwa mwaliko wa UWABA kwa mara ya pili, mara ya kwanza ikiwa ni Oktoba mwaka jana. Kutokana na mafanikio makubwa yaliyashuhudia katika msafara wa mwaka jana, tulipopata mwaliko na safari hii tuliupokea kwa kuhamasika sana.

Ndugu Mgeni Rasmi, usafiri wa baiskeli una faida nyingi sana kwa maisha ya binadamu zikiwemo; kutunza mazingira kwani ni usafiri usiotumia nishati ya mafuta ambayo matumizi yake huchangia sana katika uharibifu wa mazingira, kupunguza msongamano wa magari barabarani, kuwahi katika shughuli za kiuchumi na kijamii, mazoezi ya mwili ambayo ni muhimu kwa afya ya binadamu, n.k.

Aidha napenda kuchukua fursa hii kuelezea majukumu ya TANROADS kwa jumuiya ya wapanda baiskeli kama UWABA na wengineo.

TANROADS ilianzishwa tarehe 1 Julai 2000 kupitia Gazeti la Serikali N. 293 la mwaka 2000 chini ya kifungu cha 3(1) cha sheria namba 30 ya 1997 kuchukua

majukumu ya kuendeleza, kutengeneza na kusimamia mtandao wa barabara kuu na barabara za mikoa wenye jumla ya kilomita 33,012 kati ya mtandao wa barabara za nchi nzima wenye kilomita 86,472. Mtandao unaobakia wenye jumla ya kilomita 53,461 ukijumuisha barabara za Wilaya, za mijini na barabara za viungo (feeder roads) ziko chini ya TAMISEMI.

Kwa mfano katika jiji la Dar es Salaam barabara zilizoko chini ya TANROADS ni New Bagamoyo, Old Bagamoyo, Morogoro, Sam Nujoma, Nyerere, Kilwa, Ohio na Mandela. Barabara zilizobakia ziko chini ya mamlaka za TAMISEMI kupitia manispaa za Dar es Salaam.

Hapa ninalotaka kusisitiza ni kuwa si barabara zote ziko chini ya Wakala wa Barabara TANROADS. Hivyo katika kuzungumzia masuala yanayohusu barabara zetu nchini, hatuna budi kuzingatia mgawanyo huo.

Katika kutekeleza majukumu yake katika barabara zilizoko chini ya mamlaka yake, TANROADS pamoja na mambo mengine inazingatia usalama wa watumiaji wa barabara, wakiwemo waendao kwa miguu, wenye magari na watumiaji wa vyombo visivyo vya moto kama vile wapanda baiskeli, maguta, mikokoteni, n.k.

Ili kuhakikisha usalama wa wasafiri watumiao vyombo visivyo vya moto, TANROADS inajitahidi kujenga njia za baiskeli na watembea kwa miguu kila tunapopanua na kuboresha barabara zetu ili kutenganisha vyombo vya moto na visivyo vya moto. Aidha TANROADS inafanya jitihada mbalimbali za kutoa elimu kwa umma juu ya matumizi bora ya barabara ili kuongeza usalama wa watumiaji wa barabara.

TANROADS pia kila inapowezekana, kulingana na uwezo wa kifedha na upatikanaji wa nafasi ya ardhi hasa kwa maeneo ya mijini, inajitahidi kujenga barabara ya huduma (service roads).

Barabara za huduma hujengwa ili kukusanya magari kutoka kwenye barabara za mitaa kwenda kwenye barabara kuu ili kuongeza uwezo wa barabara kuu na kudumisha usalama wa watumiaji wa barabara. Tofauti iliyopo kati ya barabara za huduma na njia za wapandabaiskeli ni kwamba barabara za huduma zina upana zaidi upatao mita 3, kwa kiasi cha kuweza kupitisha magari; wakati njia za wapanda baiskeli na watembea kwa miguu ni njembamba na zina upana kati ya mita 1.5 na 2 ambao huwezesha watumiaji kupishana lakini hauruhusu magari kupita.

Ni muhimu kuweza kutambua aina hizo za barabara za huduma na zile zinazojengwa mahususi kwa matumizi mengine ili watumiaji wa barabara kama UWABA muweze kutumia barabara ipasavyo kwa usalama wenu na kuchangia katika matumizi sahihi ya barabara husika.

TANROADS pia ina jukumu la utunzaji wa mazingira katika majukumu yake ya matengenezo na ujenzi wa barabara. Tunatoa rai kwa UWABA pamoja umma wote uliojitokeza katika hafla hii leo, kwa pamoja tuendelee kulivalia njuga suala la utunzaji wa mazingira ili tuweze kuinusuru nchi yetu na athari za tabia nchini kwa maslahi yetu na vizazi vyetu vijavyo.

Nichukue fursa hii pia kutoa rai kwenu msaidiane na TANROADS na vyombo vingine vyenye mamlaka, katika kutunza vifaa vya barabarani kama vile alama za barabarani, taa za barabarani (street lights), taa za kuongozea magari (traffic lights) n.k. Vifaa hivi ni muhimu katika kuchangia usalama barabarani na matumizi bora ya barabara zetu.

Mwisho TANROADS inatoa wito kwa watumiaji wote wa barabara, waendeshao magari, watembea kwa miguu na wapanda baiskeli kulinda usalama wao na usalama wa watumiaji wengine wa barabara.

ASANTENI SANA!